

**MBINGA FARMERS CO- OPERATIVE UNION LTD**  
**REG NO, 5556**  
**BOX 100 – MBINGA**  
**Email: mbifacultd@gmail.com**

---

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

*chama kikuu cha ushirika cha Mkoa wa Ruvuma (MBIFACU LTD) chenye namba ya Usajiri 5556 kilichoanzishwa kwa dhumuni la kutoa huduma bora kwa wakulima wa zao la kahawa wa Wilaya ya Mbanga Mkoani Ruvuma.* Ili kuhakikisha kinaendelea kutoa huduma kwa wanachama wake, MBIFACU Ltd kinatangaza nafasi ya kazi (1) moja ya Mkaguzi wa Ndani .

**1.0 MKAGUZI WA NDANI**

**1.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe na elimu isiyopungua shahada ya kwanza au stashada ya juu ya uhasibu kutoka katika Chuo cha Ushirika Moshi au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali;
- Awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu (3) katika nafasi aliyoomba;
- Awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika kwa usafaha lugha ya Kiswahili na kiingereza;
- Awe na uwezo wa kutumia kompyuta na misumo mbalimbali ya kifedha pamoja na sifa nyingine kadiri itakavyoonekana inafaa;
- Awe mbunisu na mwenye bidii katika kazi bila kusimamiwa;
- Awe na sifa ya uadilisu;
- Awe hajawahi kufukuzwa kazi kwa tuhuma za upotevu wa fedha au kupatikana na makosa ya jinai;
- Awe na umri usiopungua miaka 25 na usiozidi miaka 45

**1.2 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kusimamia utendaji wa kazi katika Idara ya Ukaguzi wa Ndani;
- ii. Kufanya ukaguzi wa mapato ya Chama na kuhakikisha matumizi yanaendana nay ale yanayoidhinishwa;
- iii. Kutoa taarifa ya ukaguzi wa fedha za chama kila mwezi, kila baada ya miezi mitatu (3) na mwisho wa mwaka kwa meneja wa chama ;

- iv. Kufanya malinganisho ya miamala ya leja kuu na hesabu za benki kila mwezi ;
- v. Kubuni mbinu za kupata mapato ya ziada kwa chama;
- vi. Kushirikiana na Mhasibu wa chama pamoja na wakaguzi wanje katika kukamilisha ukaguzi wa hesabu za chama;
- vii. Kufanya ukaguzi AMCOS za chama kikuu cha ushirika MBIFACU Ltd;
- viii. Kutoa taarifa ya ukaguzi huo kwa viongozi wa AMCOS na viongozi wa Bodi ya chama kikuu cha ushirika MBIFACU Ltd;
- ix. Kuwa mshauri wa shughuli za kihasibu kwenye AMCOS na chama kikuu cha Ushirika (MBIFACU Ltd;
- x. Kutoa elimu juu ya utunzaji bora wa vitabu vya fedha kwa mameneja na wahasibu wa AMCOS na chama kikuu cha Ushirika (MBIFACULtd;
- xi. kutekeleza majukumu mengine atakayopangiwa na Meneja Mkuu wa Chama.

### **1.3 MSHAHARA**

Kiwango cha mshahara kitakuwa kwa mujibu wa viwango vya Chama Tshs 500,000.0

### **1.4 MASHARTI YA NAFASI YA KAZI**

- i. waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania
- ii. waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa,
- iii. waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojoitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika;
- iv. barua iandikwe kwa mkono na kusainiwa;
- v. maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya tualuma, maelezo binafsi na nakala za vyeti vya kuhitimu masunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika (Professional Certificate from respective Board);
- vi. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**)  
**HAVITAKUBALIWA;**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA NA NACTE);
- viii. Mwombaji atakayeitwa kwenye usaili aje na vyeti halisi siku ya usaili;
- ix. Mwombaji atajigharamia mwenyewe siku ya usaili;
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria;
- xi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili  
**HAYATAFIKIRIWA;**

*Barua ya maombi landikwe kwa mkombo na mwombaji mwenzewe.*

Tangazo hili limetolewa tarehe 21/5/2021 Saa 2.00 Asubuhi na mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 21/06/2021 saa 10.00 Jioni.

Maombi yote yatumive au yaletwe Ofisi ya MBIFACU LTD, kwa amani ifuatayo hapa chini.-

**MENEJA MKUU**

**MBIFACU LTD**

**S.L.P 100**

**MBINGA.**

Email: [mbifacultd@gmail.com](mailto:mbifacultd@gmail.com)

